

Vichwa vya Habari:

Uchumi wa Dunia Wakabiliwa na Mtihani Mkubwa wa Dhiki Mwaka 2023

Familia za Kiingereza Zala CHAKULA CHA MIFUGO

Mgogoro wa Kiuchumi wa Pakistan Wayalazimisha Masoko Kufunga Mapema

Maelezo:

Uchumi wa Dunia Wakabiliwa na Mtihani Mkubwa wa Dhiki Mwaka 2023

Ukweli kwamba ulimwengu haukupata mgogoro wa kifedha wa kimfumo mnamo 2022 ni muujiza mdogo, kutokana na kupanda kwa mfumko wa bei na viwango vya riba, bila kutaja ongezeko kubwa la hatari ya kijiografia na kisiasa. Lakini kutokana na deni la umma na la kibinafsi kupanda hadi kufikia viwango vya juu wakati wa enzi ya sasa ya viwango vya chini vya riba, na hatari ya kushuka kwa uchumi kuwa kubwa, mfumo wa kifedha wa kilimwengu unakabiliwa na mtihani mkubwa wa dhiki. Mgogoro katika uchumi ulioendelea - kwa mfano, Japan au Italia - utakuwa mgumu kuudhibiti. Kweli, udhibiti mkali umepunguza hatari kwa sekta kuu za benki lakini hiyo imesababisha tu hatari kuhama mahali pengine katika mfumo wa kifedha. Kupanda kwa viwango vya riba, kwa mfano, kumetia shinikizo kubwa kwa makampuni ya hisa ya kibinafsi ambayo yalikopa sana kununua mali. Sasa, huku nyumba na mali isiyohamishika ya biashara zikiwa kwenye ukingo wa kushuka kwa kasi, kwa kudumu, kuna uwezekano mkubwa baadhi ya makampuni hayo yataanguka. Katika hali hiyo, benki za msingi ambazo zilitoa kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya ununuzi wa mali isiyohamishika zinaweza kuwa matatani. Hilo bado halijatokea, kwa kiasi fulani kwa sababu makampuni yaliyodhibitiwa kidogo yako chini ya shinikizo dogo la kuweka alama kwenye hesabu zao za soko. Lakini tuseme viwango vya riba vinasalia kuwa juu kwa ukaidi hata wakati wa mdororo (uwezekano dhahiri tunapoondoka katika enzi ya viwango vya chini zaidi). Katika hali hiyo, makosa mengi ya malipo yanaweza kufanya iwe vigumu kudumisha muonekano.

Masaibu ya hivi majuzi ya kifedha ya Uingereza yanaonyesha aina ya mambo yasiyojulikana ambayo yanaweza kutokea wakati viwango vya riba vya kimataifa vinapoongezeka. Ingawa waziri mkuu wa zamani Liz Truss alichukua lawama zote kwa kukaribia kudorora kwa soko la dhamana na mfumo wa pensheni wa nchi yake, mhusika mkuu aligeuka kuwa wasimamizi wa hazina ya pensheni ambao kimsingi walicheza kamari kuwa viwango vya riba vya muda mrefu havitapanda haraka sana. Japan, ambako benki kuu imeweka viwango vya riba kuwa sifuri au hasi kwa miongo kadhaa, inaweza kuwa nchi iliyo hatarini zaidi ulimwenguni. Kando na viwango vya chini kabisa, Benki Kuu ya Japan pia imejikusisha na udhibiti wa muundo wa mavuno, ikiweka dhamana za miaka mitano na 10 kwa takriban sifuri. Kwa kuzingatia ongezeko la viwango vya riba halisi duniani kote, uchakavu mkubwa wa yen, na shinikizo la juu la mfumko wa bei, hatimaye Japan inaweza kuondoka katika enzi yake ya karibu sifuri. Viwango vya juu vya riba vitaweka shinikizo kwa serikali ya Japan mara moja, kwani deni la nchi linafikia 260% ya Pato la Taifa. Ikiwa mtu angeunganisha mizania ya BOJ, takriban nusu ya deni la serikali lililonunuliwa na sekta ya kibinafsi ni kwa ufanisi katika vifungo vya muda mfupi. Ongezeko la kiwango cha riba cha 2% linaweza kudhibitiwa katika mazingira ya ukuaji wa juu, lakini matarajio ya ukuaji wa Japan yatapungua kadiri viwango vya riba halisi vya muda mrefu vikiendelea kuongezeka. Italia ni mfano mwingine wa hatari iliyofichika. Kwa njia nyingi, viwango vya riba vya chini sana vimekuwa gundi inayoshikilia eurozone pamoja. Dhamana ya wazi kwa deni la Italia, kulingana na ahadi ya rais wa zamani wa Benki Kuu ya Ulaya Mario Draghi ya 2012 ya kufanya "chochote kinachohitajika," ilikuwa nafuu wakati Ujerumani inaweza kukopa kwa viwango sifuri au hasi. Lakini kupanda kwa kasi kwa kiwango cha riba mwaka huu kumebadilisha hesabu hiyo. Leo, uchumi wa Ujerumani unaonekana zaidi kama ulivyokuwa mwanzoni mwa miaka ya 2000, wakati wengine waliuita "mtu mgonjwa wa Ulaya". Na ingawa Ulaya ni ngeni kwa viwango vya chini kabisa, unapaswa kuwa na wasiwasi kwamba wimbi endelevu la kubana fedha linaweza, kama ilivyo kwa Japan, kufichua mifuko mingi ya hatari. [Chanzo: The Guardian]

Urasilimali kwa mara nyingine tena umeileta dunia kwenye kilele cha janga la kiuchumi ambalo litadumaza janga la kifedha duniani la mwaka 2008. Suluhisho pekee la mizunguko hii haribifu ya kiuchumi ni Uislamu. Uislamu haukubaliani na ukuaji mkubwa unaochochewa na mikopo ambapo uchumi uko chini ya uangalizi pekee wa matajiri wakubwa kutengeneza pesa kwa gharama ya kila mtu mwengine.

Familia za Kiingereza Zala CHAKULA CHA MIFUGO

Mfanyikazi mmoja wa jamii aliye na uzoefu wa miaka 20 alisema watu wanalazimika kula chakula cha mifugo huku wengine wakipasha moto chakula chao kwenye radiators kutokana na gharama inayoendelea ya shida ya maisha. Mark Seed, ambaye anaongoza mradi wa chakula cha jamii huko Trowbridge, Cardiff, anahimiza watu katika kaya zinazotatizika kupewa usaidizi wa kutosha, hata wakati hawaonekani katika maeneo yanayohusiana na umaskini. Anapendekeza kuwa kutokana na kupanda kwa mfumko wa bei sera zinapaswa kulenga watu, sio maeneo. Akizungumzia matukio ambayo ameshuhudia, aliiambia BBC Wales: 'Bado ninashtushwa na ukweli kwamba tuna watu ambao wanakula chakula cha mifugo,' alisema. '[Kuna] watu ambao wanajaribu kupasha moto chakula chao kwenye radiator au mshumaa. 'Hizi ni aina za hadithi za kushtua ambazo kwa hakika ni ukweli.' Alijadili jinsi watu hawalipwi vya kutosha kumudu mahitaji ya kimsingi na mahitaji muhimu ambayo wote wanapaswa kupata. Pantry, ambako Bw Seed anafanya kazi, ni kituo kinachofadhiliwa na Wakfu wa Jumuiya ambacho kinalenga kupunguza umaskini wa chakula huko Cardiff na kutoa chakula cha bei nafuu na mahitaji ya familia kwa zaidi ya wenyeji 160. Huku gharama ya maisha inavyoendelea, takwimu za hivi majuzi zilionyesha mfumko wa bei ukipanda hadi kiwango kipya cha juu cha miaka 41 cha asilimia 11.1 - huku wataalamu wakionya juu ya hali mbaya zaidi ijayo. ONS ilikusudia kwamba bila Serikali kutoa ruzuku kwa bili za nishati wakati wa miezi ya baridi, CPI ingeweza kuwa juu kama asilimia 13.8 na wataalamu walionya Uingereza inakabiliwa na 'mchanganyiko hatari' wa kushuka kwa uchumi na kupanda kwa bei. Kupanda kwa gharama za chakula na nishati kumetajwa kuwa sababu kuu ya ongezeko la hivi punde, huku Afisi ya Takwimu ya Kitaifa ikikadiria kuwa familia ya wastani ya Uingereza sasa inalipa asilimia 88.9 zaidi ya kupasha joto na kuwasha taa kuliko mwaka jana. Takwimu mpya za mfumko wa bei zinaonyesha kuwa bei ya bidhaa kuu za familia kama vile maziwa, siagi, jibini, nyama na mkate iliongezeka hadi asilimia 42 mwezi uliopita - viwango vya juu zaidi tangu 1980. [Chanzo: Daily Mail]

Urasilimali huwawezesha matajiri wakubwa kufanya wizi wa mchana wakati wa mgogoro wa gharama ya maisha kwa kuhamisha gharama kwa raia. Uislamu unahakikisha kwamba kila mwanadamu katika sayari hii ana haki ya chakula, mavazi, na makaazi katika utabikishaji ndani ya Dola ya Kiislamu. Zaidi ya hayo, Uislamu unakataza uhamishaji wa mali kutoka kwa raia kwenda kwa matajiri wakubwa, ambapo daima huzunguka katika mikono ya watu wachache wanaoitumia kuhifadhi maslahi yao tu.

Mgogoro wa Kiuchumi wa Pakistan Wayalazimisha Masoko Kufunga Mapema

Serikali ya Pakistan imeamuru vituo vya biashara na masoko kufungwa mapema kila siku huku nchi hiyo ikikabiliwa na mzozo wa kiuchumi. Waziri wa ulinzi Khawaja Asif anasema hatua hizo zitaokolea taifa hilo la Asia Kusini karibu rupia za Pakistan 62 bilioni (\$274.3m; £228.9m). Pakistan inazalisha umeme wake mwingi kwa kutumia nishati ya mafuta ya kisukuku kutoka nje. Bei ya nishati ya kimataifa ilipanda mwaka jana, na kuweka shinikizo zaidi kwa fedha za nchi hiyo ambazo tayari zimepungua. Ili kulipia uagizaji wa nishati hiyo nchi inahitaji fedha za kigeni, hasa dolari za Marekani. Serikali ya Pakistan ilikuwa na \$11.7 bilioni ya fedha za kigeni zilizopatikana mwezi uliopita baada ya akiba yake kushuka kwa takriban 50% mwaka jana. Hiyo inatosha tu kugharamia takriban mwezi mmoja wa uagizaji wa bidhaa zote za nchi, nyingi zikiwa ni nishati. Wakati huo huo, uzalishaji wa banka za umeme usio na ufanisi utapigwa marufuku kuanzia mwanzo wa Julai. "Baraza la mawaziri la kifederali limeidhinisha mara moja utekelezaji wa Mpango wa Kuhifadhi Nishati," chama tawala cha Pakistan Muslim League-N (PML-N) kilisema kwenye Twitter. Taifa hilo lenye watu milioni 220 limekuwa likijitahidi kwa miaka mingi kuleta utulivu wa uchumi wake. Mnamo 2019 Pakistan ilipata dhamana ya \$6 bilioni kutoka kwa Mfuko wa Fedha wa Kimataifa, huku Agosti mwaka jana ikipokea \$ 1.1 bilioni zaidi. Serikali pia inajadiliana na IMF kuhusu kucheleweshwa kutolewa kwa \$1.1 bilioni nyingine ya pesa za uokoaji. Fedha za Pakistan pia ziliathiriwa mwaka jana na mafuriko makubwa yaliyoikumba nchi hiyo. Mnamo Oktoba Benki ya Dunia ilikadiria kuwa mafuriko hayo yalisababisha uharibifu wa \$40 bilioni kwa nchi hiyo. [Chanzo: BBC]

Haijalishi tena ni chama gani cha siasa kilicho madarakani au kama jeshi linatawala au la. Uongozi mzima hauna masuluhisho yoyote ya kiuchumi ya kukomesha kudorora kwa uchumi wa Pakistan. Ni kwa kusimamishwa tena Khilafah Rashida kwa njia ya Utume pekee ndiko kunakoweza kurudisha ubwana wa kiuchumi nchini Pakistan na kukomesha kabisa uingiliaji wa dola za kigeni na taasisi zao katika masuala ya kiuchumi ya Pakistan.